

Uchukuzi yaja na bajeti ya tril 2.9/-

Na Anastazia Anyimike,
Dodoma

SERIKALI inatarajia kutumia Sh trilioni 2.872 kutekeleza miradi ya maendeleo na shughuli za Wizara ya Uchukuzi na taasisi zake katika Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Waziri wa Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa amesema fedha hizo ni sawa na asilimia 4.6 ya bajeti yote ya serikali ya Sh trilioni 62.334.

Profesa Mbarawa alisema hayo katika hotuba ya kufungua Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi iliyosomwa na Naibu Waziri, David Kihenzile jijini Dodoma jana.

Profesa Mbarawa alisema kikao hicho ni muhimu na kinatoa fursa ya kupitia utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka 2025/2026 na kujadili mpango wa mwaka 2026/2027 kwa kushirikisha wafanyakazi.

Alisema serikali inaendelea kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Uchukuzi ya Mwaka 2003, ambapo mchakato wake unatarajiwa kukamilika mwaka huu ili kuendana na mahitaji ya sasa ya sekta hiyo.

Profesa Mbarawa alisema serikali imeendelea na kuboresha mfumo wa kisheria kwa kurekebisha sheria mbalimbali zikiwamo Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), Sheria ya Bandari na Sheria ya Leseni za Usafirishaji ili kuongeza ufanisi, usalama na udhibiti wa huduma za uchukuzi.

Aidha, alisema pia miradi ya kimkakati imeendelea

kutekelezwa kwa mafanikio ikiwamo ujenzi wa Reli ya Kisasa (SCR), ambapo huduma za abiria na mizigo kati ya Dar es Salaam na Dodoma zinaendelea kutolewa.

Profesa Mbarawa alisema serikali pia imeendelea kuimarisha Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) ambayo kwa sasa ina jumla ya ndege 16 zinazotoa huduma, pamoja na kuboresha huduma za bandari kupitia ushirikiano na sekta binafsi hususani Bandari ya Dar es Salaam.

Kuhusu usafiri wa majini, alisema serikali imekamili-sha ujenzi wa meli ya MV New Mwanza katika Ziwa Victoria na MT Sangara katika Ziwa Tanganyika, huku ukarabati wa meli nyingine ukiendelea.

Akizungumzia mafanikio ya mwaka 2025/2026, Profesa Mbarawa alisema Shirika la Reli Tanzania (TRC) limeanza kujitegemea kifedha na hivyo kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali Kuu.

Alisema wizara hiyo itaendelea kutenga fedha za ufuatiliaji na tathmini ya utendaji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Akitoa maelezo yake, Kihenzile alisema ni vyema watumishi wakajipanga kutekeleza bajeti hiyo ambayo ni ya kwanza kuelekeza utekelezaji wa Dira 2050.

Awali, Mwenyekiti wa Baraza na Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi, Profesa Godius Kahyarara alisema miradi ya maendeleo inayotekelezwa na wizara inaendelea vizuri, huku akisisitiza kuwa utegemezi wa ruzuku kwa taasisi za wizara hiyo imepungua.